# Nguvu ya **Ukwasi** Katika Kueneza **Ufalme**



**James Kalekwa**

# NGUVU YA UKWASI KATIKA KUENEZA UFALME

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Tabaruku.......................................................................... 4

Salamu na Utangulizi.......................................................... 5

Sura ya Kwanza:.................................................................. 7

*Dhana ya Nguvu na Utendaji wake*.................................... 7

Adui hutiishwa, hukabiliwa na huitikia WINGI WA NGUVU.......................................................................... 9

SURA YA PILI:.................................................................... 12

*Utumishi kwa Mali*.............................................................. 12

Sura ya Tatu:........................................................................ 15

*Kuyabariki Maisha ya Wengine*.......................................... 15

SURA YA NNE:..................................................................... 18

*Kufadhili kazi ya Mungu na wahudumu wa injili.*............. 18

SURA YA TANO:................................................................... 21

*Kulinda Ushuhuda wa Mwamini*......................................... 21

SURA YA SITA:..................................................................... 25

*Kuimarisha Kazi ya Mungu*................................................. 25

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarif aya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anvyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani

huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2023
Dodoma, Tanzania

## Sura ya Kwanza:

*Dhana ya Nguvu na Utendaji wake*

> *"Bali utamkumbuka BWANA, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo."* **Kumbukumbu la Torati 8:18**

Kwa nini Mungu anataka UWE NA NGUVU YA FEDHA NA UONGEZEKE KATIKA HIYO?

NGUVU ITAKAYOKUFANYA KUWA MTU WA MATOKEO/MGUSO (IMPACT).

Kuhusu Nguvu:

1. Nguvu hupimika na/au zina kiwango (nyingi au chache)

*"...kwa ajili ya WINGI wa nguvu zako, Adui zako watakuja kunyenyekea mbele zako."*
Zaburi 66:3

*"Ukizimia siku ya taabu, Nguvu zako ni CHACHE."*
Mithali 24:10

Kuna mazingira, hali, nyakati zitakuja kwenye maisha yako ili ufahamu kiwango cha nguvu... Hapa ninamaanisha ujifahamu wewe mwenyewe mfano: Siku ya taabu. Siku ya namna hii haipo kukuangamiza bali kukujulisha una nguvu kiasi gani.

Vile vile, kuna nafsi (katika roho au katika mwili) zitakukabili ili ufahamu kiwango/kipimo cha nguvu zako. Kuna nafasi huja na mamlaka nyingi, manufaa mengi na majaribu mengi. Kuna majukumu ambayo yamebeba ndani yake uwezekano mkubwa wa kulaumiwa. Kuna majukumu yamebeba ndani yake uwezekano mkubwa wa kusalitiwa. Pia, kuna majukumu ambayo yamebeba mamlaka kubwa sana ndani yake kiasi kwamba ukikosa nguvu za kujichukua katika mamlaka hiyo, unaweza kufanya mambo yasiyokustahili kuyafanya.

Yote kwa yote,

Siku ya taabu huitikia, hutiishwa, hukabiliwa kwa WINGI WA NGUVU. Kinyume cha hapo (yaani kuzimia) ni kiashiria cha NGUVU chache.

Adui hutiishwa, hukabiliwa na huitikia WINGI WA NGUVU.

Kuna aina fulani ya matokeo utayapata kwa kuwa na aina fulani ya nguvu.

> *"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."*
> Matendo ya Mitume 1:8

> *"...hujifanyizia njia kwa nguvu kati ya silaha, wala hawaachi kuifuata njia yao."*
> Yoeli 2:8

Adui anaelewa lugha ya NGUVU TU, si pungufu ya hapo!

Swali kubwa ambalo nimejihoji muda mrefu kila nikisoma andiko linaloongoza kitabu hiki, Kumbukumbu la Torati 8:18… kwa nini Mungu anatoa NGUVU za kupata utajiri? Si watu waende tu wawe matajiri? Halafu ni kwa nini Mungu anaonyesha kuhusika na kuwa mdau wa karibu sana wa watu wake kupata nguvu ya utajiri? Mbona kama Mungu ana "vested interests" kwenye utajiri wetu wanadamu. Kwani Yeye unamuhusu nini?

Kuna baadhi ya maswali, kwa sababu kadhaa, sitayaandika hapa. Hata hivyo yote pamoja na yaliyotangulia yalinipelekea kuanza kusoma neno la Mungu kwa utafiti. Nilijifunza jambo hili mapema… nikiona Mungu amesema jambo kwenye neno lake ninapaswa nilitafiti mpaka nimuelewe kisha nigeuze yawe ni maombi na utendaji wangu. Sijidhanii ya kwamna nimefika lakini ninajua ya kwamba sipo gizani. Kuna mahali nipo na ninaenda!

Kwa nini ninahitaji nguvu kuwa tajiri? Tena kwa nini ninahitaji nguvu za Mungu kuwa tajiri? Nikagundua mambo mengi kwenye maswali hayo.

Ni vyema ujue neno la Mungu linapozungumzia utajiri kwenye andiko hili linasema "wealth" na siyo "riches". Tafsiri sahihi ya Kiswahili ya wealth ni ukwasi na si utajiri. Kwa hiyo, ninahitaji ukwasi kumbe na si utajiri!

Kwa kifupi, utajiri ni kuwa na upaji (supply) ya kuyatosha maisha yako na wanaokuhusu kwa ukaribu wakati ukwasi ni kuwa na upaji zaidi yako, zaidi ya

wanaokuhusu, zaidi ya muda wako duniani na zaidi ya vizazi vyako… Hiyo inahitaji uwe na nguvu mpendwa.

Kwenye sura zinazofuatia za kitabu hiki, nitawekeza muda mwingi kujibu swali hili la kwanini ukwasi. Ambalo ndani yake utagundua linakuonyesha sababu gani Mungu yuko interested na wewe kuwa mkwasi.

# SURA YA PILI:

*Utumishi kwa Mali*

Mali ni nyenzo muhimu sana mikononi mwa mwamini kwa ajili ya kumtumikia Mungu. Ufahamu huu ukiingia ndani mwako kuna namna utautazama ukwasi na kuna namna utautazama utumishi.

> *25 Musa akasema, Ni lazima utupe mikononi mwetu na wanyama wa dhabihu na wa sadaka za kuteketezwa,* ***ili tupate kumchinjia Bwana Mungu wetu dhabihu.***
>
> *26 Makundi yetu pia watakwenda pamoja nasi; hautasalia nyuma hata ukwato mmoja;* ***kwa maana inampasa kutwaa katika hao tupate kumtumikia Bwana,*** *Mungu wetu; nasi hatujui, hata tutakapofika huko,* ***ni kitu gani ambacho kwa hicho inatupasa kumtumikia Bwana.***
>
> Kutoka 10:25-26

Ili upate kumtumikia na kumwabudu kwa MALI zako.

Kama ilivyo kuimba, kunyanyua mikono, kupiga magoti, kupiga makofi n.k ni namna ya kuwasilisha (express) ibada yako kwa BWANA; Ndivyo na MALI ilivyo!

Kuna ufunuo ambao Musa anatufunulia hapa kwa kutumia neno linaloonyesha hali ya sharti… hali ya ulazima… hali ya kupoteza uhiyari wetu linapokuja swala la kumtumikia BWANA. Imetupasa! Maana yake ni lazima na hakuna mjadala na yeyote katika hilo.

Mambo yoyote ambayo "imepaswa" huwa yanakuacha wewe uamue kuwa ndani au nje na huwa hakuna namna utayaathiri.

Neno la Mungu linatuonyesha Mungu anaweza akataka chochote kutoka kwenye mali zetu ili tuweze kumtumikia kwazo. Ndiyo maana Musa anasema "hatujui…" akimaanisha ya kwamba Mungu anaweza kuitisha chochote kutoka kwenye hazina zetu. Ni lazima kiwepo kwanza!

Halafu ningependa ugundue ya kwamba watu hawa wa kale walikuwa na ufunuo tayari ya kwamba Mungu hatumikiwi kwa mikono mitupu tu! Mungu wetu hutumikiwa kwa mali alizotubariki nazo.

Kama unataka kumtumikia Bwana, hakikisha una "vifaa" vya kumtumikia Bwana – UKWASI.

Ninakumbuka mwaka mmoja tulipoanza kuwafundisha watoto wetu kutoa sadaka tena kiwango fulani cha sadaka. Mpendwa wetu mmoja aliona tunawapatia ile sadaka. Akafanya hesabu za kujumlisha na akaona zile sadaka zingeweza kufanya mambo makubwa na ya ajabu sana kwenye maisha yake. Siku kadhaa baadaye aliamua kujikaza na kuelezea namna gani "tunawaharibu" watoto wetu kwa kuwashikisha fedha "nyingi" wakatoe sadaka. Ilitushangaza kiasi. Lakini baadaye ilibidi tumfunulie maandiko kumuonyesha kile tunachokijenga kwenye mioyo ya watoto wetu. Kuwa na ukwasi na kuutumia kumtumikia Mungu bila kuzuilia kitu!

## Sura ya Tatu:

*Kuyabariki Maisha ya Wengine*

Kwanini Mungu anataka UWE NA NGUVU YA FEDHA NA UONGEZEKE KATIKA HIYO.

> *"Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe,* ***apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.****"*
>
> Waefeso 4:28

Ili uwe mikono ya Mungu hapa duniani kuyahudumia mahitaji ya watu wengine. Unajua hapa duniani kuna wahitaji. Yesu alisema masikini hawatakosa; Neno la Mungu limesema kuhusu kuwahurumia masikini.

> "Kwa maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi; lakini mimi hamnami siku zote." Mathayo 26:11
>
> "Amhurumiaye maskini humkopesha BWANA; Naye atamlipa kwa tendo lake jema." Mithali 19:17

Uchaguzi ni wako- kuwa upande wa kumgawia muhitaji; au upande wa kugawiwa!

Sasa, neno la Mungu linaonyesha ya kwamba mwamini ambaye alikuwa na tabia ya uibaji, anapaswa kutoendelea na tabia hiyo kwa kuwa ni mwamini. Na kuna maelekezo ya kufanya baada ya kubadili uelekeo. Afanye kazi kwa bidi ajipatie mali zake mwenyewe. Hapa utagundua ya kwamba mtume Paulo akivuviwa na Rogo Mtakatifu anaeleza sababu moja wapo ya mwamini kujipatia kipato chake mwenyewe ni ili awezekumsaidia muhitaji.

Mwamini ndiye mikono ya Mungu hapa duniani katika kumsaidia muhitaji.

Kuna kweli moja nilifundishwa ambayo haijawahi kuondoka moyoni mwangu. Niliambiwa ya kwamba namna bora na ya kwanza ya kuwasaidia wahitaji na masikini ni mimi kutokua mmoja wao; kupunguza idadi ya wahitaji na masikini… kisha baada ya hapo ni mimi

kujipatia ukwasi mwingi kiasi cha kuweza kukutana na mahitaji ya mtu masikini. Huwezi kumsaidia masikini na muhitaji kutoka kwenye umasikini na uhitaji!

Ni sawa na kusema. Kama hupendi sana ukwasi au unaona ni hali ya kujiinua na kujikweza. Basi, usiutafute kwa ajili yako bali wawazie masikini na wahitaji. Utake na utafute kwa ajili yao!

Kwa uelewa huo huwa ninafikia hitimisho ya kwamba watu wasiopenda ukwasi ni watu wabinafsi sana. Wanajiwazia wao na matamanio yao kibinafsi. Rafiki, wawazie watu wengine!

Mungu anataka akutumie kama mikono yake kuonyesha upendo na ufadhili wake kwa wanadamu!

Kama kuna watu wanapaswa kuwa wakwasi basi ni waamini. Ni kwa ajili ya kuwa mfereji wa Mungu hapa duniani kuwabariki wanadamu kwa namna mbalimbali kupitia mali.

Ukiuchukia na/au kukoosa ukwasi ujue fika kabisa ya kwamba umempunguzia Mungu machaguo ya kuwasaidia wahitaji na masikini!

## SURA YA NNE:

*Kufadhili kazi ya Mungu na wahudumu wa injili.*

Kwa nini Mungu anataka UWE NA NGUVU YA FEDHA NA UONGEZEKE KATIKA HIYO. Ni ili uweze kuifadhili kazi ya injili na watumishi wa kazi hiyo.

*"**Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe**? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?"*

1 Wakorintho 9:7

*"Tena **wahubirije, wasipopelekwa**? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!"*

Warumi 10:15

Ni kweli ya kwamba wokovu ni bure; na ni kweli pia ya kwamba injili ni gharama! Ili injili ienezwe kwenye maeneo mbalimbali ya kijiografia, kwa vizazi

mbalimbali, na kwa mataifa na makundi tofauti. Gharama ya fedha na mali zinahitajika.

Kwa ukosefu wa ukwasi, makundi ya watu hayajafikiwa. Si kwa sababu injili ni dhaifu au kwamba injili ni uongo bali ni kwa sababu ya ukosefu wa ukwasi.

Mungu anataka uwe mkwasi ili utumie rasilimali kuiwezesha kazi ya Mungu kukua na kuenea – kufikia idadi kubwa ya watu na eneo kubwa kijiografia kwa wepesi.

Kwa ufahamu huo, huwa ninafikia kwenye hitimisho ya kwamba watu wanaochukia ukwasi tena kwa kuhalalisha na rejea za kidini ni maadui wa msalaba… hawataki kazi ya injili ienee kwa nguvu.

Mtu anayempenda Bwana Yesu na anawapenda watu wa Mungu vizuri atakuwa na shauku kuu ya ukwasi kwa kuwazia kazi ya Mungu.

Kwa muundo aliouweka Mungu mwenyewe ni kwamba uendeshaji wa kazi ya injili kifedha hufanywa na wanufaika wa injili husika. Lakini pia uwezeshaji wa askari wa mstari wa mbele kwenye jeshi la Bwana Yesu.

Hakuna vita ambayo huendeshwa kwa gharama za askari yeyote… duniani kote!

Kwa mfano, hii vita ya injili inapaswa kuwa redioni, mitandaoya kijamii, televisheni, machapisho ya namna mbalimbali, mikutano ya hadhara, semina, ujenzi wa makanisa kila eneo… Hayo yote yanahitaji ukwasi!

Ninakuombea kwa Bwana Yesu upate ukwasi mwingi kiasi cha kulipia gharama za uratibu na uendeshaji wa vita Imani! Pokea utele wa ukwasi na mali ili umuwezeshe askari mmoja wa mstari wa mbele katika vita hivi vya injili.

## SURA YA TANO:

*Kulinda Ushuhuda wa Mwamini*

Kwanini Mungu anataka UWE NA NGUVU YA FEDHA NA UKUE KATIKA HIYO. Ni ili uweze kuulinda ushuhuda wako mbele ya watu wasioiamini injili.

Kwenye madarasa mbalimbali ya vijana nilipofundisha kuhusu kisa cha kanisa la Thesalonike, huwa ninaeleza changamoto kubwa ambayo walikuwa nayo watu hawa wa Mungu. Baada ya injili ya mtume Paulo kuwafikia nao wakaipokea na kuamini. Kuna watu malaghai waliojiita kuwa ni mitume, walipita Thesalonike wakaanza kufundisha ya kwamba Yesu atarudi "hivi karibuni".

Fundisho hili lilizua taharuki mwiongoni mwa jamii ya waamini kiasi cha kusababisha wengi kuachana na kazi zao za mikono na kuanza kumngojea Bwana kanisani; na wengine wakaanza kujishughulisha na mambo ya waamini wengine ili tu wajipatie chakula. Badala ya

kuangalia mambo ya nyumba zao… kujali miji yao; Wao wakachagua kutojali miji yao na kujifanya wanajali miji yaw engine ili tu wajipatie chakula. Kwa sasa unaweza kutumia neno "chawa". Yaani watu ambao wako radhi kufanya chochote kwa ajili ya watu wengine kumbe wakiwa wamelenga kujipatia fedha. Ndivyo walivyokuwa na watu wa Thesalonike!

Jambo hili lilizaa taharuki kanisani kiasi kwamba mtume Paulo aliandika nyaraka za kanisa la Thesalonike kwa ukali ili kukemea tabia ya uvivu miongoni mwa waamini. Hebu tuyasome maandiko yanasemaje.

> *"Basi twawaagiza hao, na kuwaonya katika Bwana Yesu Kristo, **watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe**."*
> 2 Wathesalonike 3:12

> *"**ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje**, wala msiwe na haja ya kitu cho chote."*
> 1 Wathesalonike 4:12

Ili uweze kuyamudu maisha yako na kukutana na mahitaji yako ya kimaisha. Usidhani Mungu anaipenda roho yako tu halafu mambo yanayohusiana na mwili

wako ameyaacha yajiendee na/au yajiendeshe menyewe tu!

Ukwasi utakusaidia kuyaweza… kuyamudu maisha yako na wanaokuhusu kwa ukaribu.

Ninakumbuka mwimbaji mmoja wa "zamani" (hiyo ni zamani yangu) anaitwa Yusto Onesmo ambaye kwa sasa ni mmishionari nchini Burundi. Kwenye wimbo wake uitwayo "Mungu wetu si kigeugeu"

Iliandika na kuimba:

> *... aliahidi hatutakosa unga,*
>
> *Kushiba kwetu ni utukufu kwake...*

Yesu anatukuzwa sana tunapotoshelezwa naye!

Usijeukadhani eti Mungu anachukia wewe ukitimiliza mahitaji yako ma watu wa karibu yako. Ukijenga nyumba nzuri… ukipata chakula kizuri na vinywaji: ukijatia mavazi mazuri nay a kupendeza… unadhani Mungu anajisikia vibaya pale wewe unapopendeza na kunawiri?

Kwa sababu ya mafundisho manyonge, kuna watu wameaminishwa ya kwamba unyenyekevu ni kuwa upungufu, kutindikiwa, kutoweza kukidhi mahitaji ya maisha yako. Unyenyekevu ni sawa na ufukara!

Mpendwa wangu, kushiba kwako, ni utukufu kwake!

Kuvaa kwako na kupendeza, ni utukufu kwake!

Kumiliki vitu vizuri na vya thamani, ni utukufu kwake!

Usijifinyilie kwenye akili za umasikini.

Jambo la pili tunaloliona kwenye kanisa la Thesalonike ni kuharibika kwa ushuhda wa wapendwa. Kuna namna ya walilidhalilisha kanisa mbele ya "walio nje" Huenda walianza kuomba-omba kwa watu wa nje; labda walitamani kuishi kma walio nje; au walishusha viwango na thamani ya wokovu ili wafananie ya walio nje.

Uhitaji ukawasababisha "wajikosee adabu" wao wenyewe! Na hicho ndicho umasikini huwafanyia watu.

Hakikisha unaulinda ushuhuda mtumishi!

## SURA YA SITA:

*Kuimarisha Kazi ya Mungu*

Kwanini Mungu anataka uwe na NGUVU YA FEDHA NA UONGEZEKE KATIKA HIYO? Ni ili alifanye imara agano lake duniani na kwenye maisha ya watu.

> *"Bali utamkumbuka Bwana, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo."*
>
> Kumbukumbu la Torati 8:18

> *"kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi."*
>
> Mathayo 26:28

Kuna agano kubwa zaidi ambalo Mungu amelifanya kwa njia ya damu ya Yesu Kristo pale msalabani. Ili agano hilo liwe imara na endelevu unahitaji ukwasi kufanya hivyo… makanisa yajengwe, semina nyingi zifundishwe, masomo yawekwe kwenye mfumo wa machapisho,

shule za BIblia zianzishwe, wamishonari wafadhiliwe, Biblia zipatikane kwa wingi, vipindi vya televisheni na radio vilivyojaa neno viongezeke, makambi ya mafundisho ya neno na Roho yafanyike kwa wingi.

Haya yote yanahitaji nguvu ya ukwasi. Unahitajika uwekezaji mkubwa sana wa "kufufuka mtu!"

Kwa wanaofahamu historia ya ulimwengu, wataelewa ya kwamba nchi ya Uturuki ilikuwa ni nchi iliyojazwa na injili na makanisa mengi yakafunguliwa… umeyasoma yale makanisa saba ya kitabu cha Ufunuo wa Yohana sura ya kwanza na ya pili? Ututuki ya wakati huo na Uturuki ya sasa, ni kama mbingu na ardhi. Kwa sasa, nchi ya Uturuki ni nchi ya kiislamu kabisa. Makanisa yote hayo yamefutwa na kusalia kama maghofu na majumba ya maonyesho kwa watalii.

Kuna nchi za Ulaya ambazo makanisa yanageuzwa kuwa majumba ya maonyesho.

Hii ni kwa sababu ya uwekezaji duni kwenye ufalme na kujiendekeza kufurahia maisha binafsi.

Mpendwa wangu, hakikisha unaimarisha agano la Mungu kwenye kizazi chako na zama zako.

NEW VINE CHURCH | Dodoma



## Kuhusu New Vine Church

New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



---

## Mahali tulipo

Swaswa, mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini

---

## Ratiba za Ibada

**Alhamis** Saa 11.15 jioni - saa 12.15 jioni
**Jumapili** Saa 3.00 asubuhi - saa 6.30 mchana

nvc_dodoma +255 769 240 777

## Kuhusu Mwandishi



Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa "Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari." [Habakuki 2:14]

## Mawasiliano na Mwandishi

wapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

- James Kalekwa
- james_kalekwa
- @MchungajiJK
- James Kalekwa

---

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia **+255-754-917-7764** (Kupiga simu, SMS na WhatsApp).